



Nini maana ya kuota mti au miti inaanguka au inakatwa?

Kibiblia Mti unawakilisha “MTU”.

> Marko 8:22 “Wakafika Bethsaida, wakamletea kipofu, wakamsihi amguse.
> 23 Akamshika mkono yule kipofu, akamchukua nje ya kijiji, akamtemea mate ya macho, akamwekea mikono yake, akamwuliza, Waona kitu?
> 24 Akatazama juu, akasema, Naona watu kama miti, inakwenda”.

Unaona hapo mstari wa 24? Miti inafananishwa na watu.


Hivyo unapoona katika ndoto Mti umeanguka nyumbani kwako, au kwenu au mahali popote,basi tafsiri yake ni kwamba kuna Mtu unayemfahamu au pengine wewe mwenyewe aidha atakwenda kufa au kushuka chini.

Na kifo hicho au kushushwa huko kunaweza kuwa kunasababishwa na shetani au Mungu mwenyewe.

Kama ni shetani, basi suluhisho ni Maombi, kwamba unapaswa uombe kwa bidii na Imani, ili roho ya mauti iondoke, na kumbuka huwezi kuivunja au kuiharibi mipango ya shetani kama wewe mwenyewe hujaokoka.

Huna budi umwamini Yesu na kuupata ufalme wa mbinguni maishani mwako ndipo uwe na mamlaka ya kubatilisha mipango yote ya Adui.

Lakini kama umeona umekatika au umeanguka na aliyeuangusha ni kama vile Mungu au Malaika wake, basi tambua kuwa ni Mungu anakwenda kukushusha chini au kukuangamiza kabisa, na hiyo mara nyingi ni kutokana na dhambi mtu anazozifanya zisizompendeza Mungu.





> 33 Saa iyo hiyo jambo hilo likatimizwa, likampata Nebukadreza; alifukuzwa mbali na wanadamu, akala majani kama ng'ombe, na mwili wake ulilowa maji kwa umande wa mbinguni, hata nywele zake zikakua, zikawa kama manyoya ya tai, na kucha zake kama kucha za ndege".

Umeona hapo?, Nebukadreza yeye hakufa kwasababu kiliachwa kisiki, lakini endapo na kisiki kingeondolewa basi angekufa kabisa.

Na Mfalme Nebukadreza, alikatwa kwasababu ya dhambi zake, na si kingine, wala hakulogwa na mtu,ni Dhambi tu ndizo zilizomsababishia kukatwa.

Vile vile kama umeota Mti wako umekatika au kuanguka, basi yachunguze maisha yako na utubu. Mungu anakupenda ndio maana kakuonesha hayo. Lengo ni ili utubu.

Na kama basi sio wewe basi unajukumu la kwenda kumweleza huyo ndugu uliyeona mti wake umekatika kwamba atubu.

Ubarikiwe.

Vitabu kwa njia ya ebook > info@ndotozangu.com